3 Yohana

Salamu

1 Mzee:
Kwa Gayo rafiki yangu, nimpendaye katika
kweli.

Gayo Anasifiwa Kwa Ajili Ya Ukarimu Wake

2 Mpendwa, naomba ufanikiwe katika mambo
yote na kuwa na afya njema kama vile roho yako
ifanikiwavyo.
3 Ilinifurahisha sana baadhi ya ndugu
walipokuja na kutueleza juu ya uaminifu wako
katika kweli na jinsi unavyoendelea kuenenda
katika hiyo kweli.
4 Sina furaha kubwa kuliko hii, kusikia
kwamba watoto wangu wanaenenda katika
kweli.
5 Rafiki mpendwa, wewe ni mwaminifu kwa
yale unayowatendea ndugu, ingawa wao ni wa-
geni kwako.
6 Wameshuhudia kuhusu upendo wako mbele
ya kanisa. Utafanya vyema ukiwasafirisha kama
inavyostahili kwa Mungu.
7 Ilikuwa ni kwa ajili ya hilo Jina waliondoka,
bila kukubali kupokea msaada wowote kutoka
kwa watu wasioamini.
8 Kwa hiyo imetupasa sisi kuonyesha ukarimu
kwa watu kama hao ili tuweze kutenda kazi
pamoja kwa ajili ya kweli.

Deotrefe

9 Nililiandikia kanisa, lakini Deotrefe, yeye
apendaye kujifanya wa kwanza, hakubali mam-
laka yetu.
10 Hivyo kama nikija, nitakumbuka matendo
yake atendayo, akitusingizia kwa maneno ya
hila. Wala hatosheki na hayo anayotusingizia,
bali pia hukataa kuwakaribisha ndugu, na hata
huwazuia wale walio tayari kufanya hivyo na
kuwafukuza watoke kanisani.

Demetrio

11 Rafiki mpendwa, usiige lile lililo baya bali
lile lililo jema. Yeyote atendaye mema atoka
kwa Mungu, bali atendaye mabaya hajamwona
Mungu.
12 Kila mtu ameshuhudia mema kuhusu
Demetrio, vivyo hivyo hata na hiyo kweli
yenyewe. Sisi pia twashuhudia mema juu yake,
nanyi mwajua kwamba ushuhuda wetu ni kweli.

Salamu Za Mwisho

13 Ninayo mambo mengi ya kukuandikia,
lakini sipendi kuandika kwa kalamu na wino.
14 Badala yake, nataraji kukuona upesi, nasi
tutaongea pamoja ana kwa ana.
15 Amani iwe kwako. Rafiki zetu walioko
hapa wanakusalimu. Wasalimu hao rafiki zetu
walioko huko, kila mmoja kwa jina lake.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™
Swahili: Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™ (Bible)

copyright © 2018 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili

Translation by: Biblica, Inc.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.
You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.
Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2021-04-12

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 1 Oct 2024 from source files dated 31 Aug 2023
9cbb05be-39f3-5d18-8b2a-4ba788541462